

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA.

Anwani ya Simu: "UCHUNGUZI"
Simu Nambari: 028-2220491/2220848
Nakushi Na: 0736-618755
Barua pepe: rbckagera@pccb.go.tz
Unapojibu tafadhali taja :



Mkoa wa Kagera
Mtaa wa Pwani
S.L.P 1138
35111 BUKOBA

13.08.2019

TAARIFA KWA UMMA

ALIYEJIFANYA AFISA MWANDAMIZI WA TAKUKURU AFIKISHWA MAHAKAMANI

Ndugu wanahabari,

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kagera kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka ya Mkoa wa Kagera leo Agosti 13, 2019 inakusudia kumfikisha Mahakamani **Bw. Bainomugisha Nsibu** kwa makosa ya kujihusisha na vitendo vya Rushwa na kujifanya Afisa wa TAKUKURU.

Bw **Bainomugisha Nsibu** ambaye ni fundi kompyuta na mfanyabiashara anayeishi maeneo ya Bunkanko-Nshambya- Bukoba mjini na mzaliwa wa Ruzinga-Misenyi anatarajiwa kufikishwa katika Mahakama ya Hakimku Mkazi Bukoba.

Bw. Bainomugisha Nsibu pia ni mshitakiwa katika shauri la jinai lenye namba **CC43/2019 (Baina Nsibu Ruta)** lililofunguliwa tarehe 20/2/2019 na TAKUKURU mkoa wa Kagera kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Mashitaka ya Mkoa wa Kagera. Shauri hili lipo katika Mahakama ya Hakimku Mkazi Bukoba ambapo katika shitaka hilo anashitakiwa kwa makosa ya kutoa taarifa za uongo chini ya kifungu cha 122 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 (R;E 2002).

Mtuhumiwa huyu leo atafikishwa Mahakamani kujibu mashitaka chini ya kifungu cha 100(b) kikisomwa pamoja na kifungu cha 35 vyote vya Sheria ya Kanuni ya Adhabu namba 16 (R;E 2002) kwa makosa ya kujifanya Afisa wa TAKUKURU ambaye alikuwa akijitambulisha kwa jina la John Joseph na kuomba Rushwa chini ya kifungu cha 15(1)(a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, namba 11/2007.

Uchunguzi uliofanywa na TAKUKURU umeweza kubaini kuwa **Bw.Bainomugisha Nsibu** pia hujulikana kwa majina ya (**Baina Nsibu Ruta**) na kwamba katika shauri la jinai lenye namba **CC 43/2019 (R VS Baina Nsibu Ruta)** lililofunguliwa tarehe 20/2/2019 alikuwa amejitambulisha kwa majina ya **Baina Nsibu Ruta**.

Uchunguzi wetu umethibitisha kuwa **Bw.Bainomugisha Nsibu** alis **Baina Nsibu Ruta** mnamo tarehe 11/4/2019 katika Manispaa ya Bukoba alijitambusha kwa mtu mmoja (**Jina limehifadhiwa**) kuwa yeye ni Afisa wa TAKUKURU aitwaye **JOHN JOSEPH** na kwamba anasimamia uchunguzi wa swala lake na hivyo alimuomba rushwa ya kiasi cha shilingi 450,000/= ili aweze kumsaidia kwa tuhuma zinazomkabili.

Ndugu wana Habari,

Sanjali na jambo hili napenda kuutahadharisha Umma wa wana Kagera kuwa makini sana kwani wameibuka matapeli ambao wamekuwa wakijifanya Maafisa wa Umma na kuwatapeli wananchi. Wimbi hili la utapeli limeongezeka sana katika kipindi hiki ambapo mapambano Dhidi ya Rushwa yameimarika . Hivyo ninawasihi muwe makini sana na mtu yeyote atakaye jitambulisha kuwa ni Mtumishi wa serikali mmuombe kitambulisho na mnapomtilia mashaka mtu yeyote basi toeni taarifa haraka katika vyombo vya Dola ikiwemo TAKUKURU.

Katika Mkoa wa Kagera mwaka 2017 tulimkamata Bwana Nyundo Mohamedi Nyundo kwa kujifanya Afisa wa TAKUKURU ambapo alifunguliwa shauri namba CC3/2017 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Bukoba na alihukumiwa kifungo cha miezi sita jela au kulipa fine na aliweza kulipa fine.

Vilevile, kwa mwaka huu tumeweza kumfikisha mahakamani Bw. **Abdul Rasu Mussa** katika Mahakama ya Wilaya ya Muleba na kumfugulia shauri la jinai namba 2/2019 tarehe 10/06/2019 kwa makosa ya kujifanya Afisa wa TAKUKURU na Afisa Usalama wa Taifa. Leo tunamfikisha mahakamani **Bw.Bainomugisha Nsibu** alis **Baina Nsibu Ruta** kwa makosa ya kujifanya Afisa wa TAKUKURU.

Hali hii inaonyesha kuwa katika mkoa wetu watu wanaojifanya maafisa wa Serikali wapo hivyo tuchukue tahadhari.

Nachukua fursa hii kuwakumbusha wote kwamba Rushwa ni adui wa haki hivyo kila mmoja wetu anawajibika kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za nchi zilizowekwa kwa maslahi mapana ya Taifa.

Hivyo nitoe wito kwa Wananchi wote kuchukua hatua mahususi pale wanapoonna kuna dalili za ukiukwaji wa sheria zetu za nchi au kuna viashiria vya uwepo wa vitendo vya rushwa, vinavyofanywa na mtu au kundi fulani la watu

Imetolewa na:

SIGNED

JOHN K.E JOSEPH

MKUU WA TAKUKURU (M)